**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO**

**SHULE YA SEKONDARI CHISANO,**
**S.L.P 164,**
**MLIMBA.**
**18/12/2020.**

**KUMB.NA.MEST/CHSS/S3199/FI2021/01.**

**MWANAFUNZI ………………………………………………**
**S.L.P ……………………………..**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHISANO JANUARI 2021**

Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Nakupongeza kwa kufaulu, ni imani yangu kuwa juhudi hizo utaziendeleza hapa shuleni. Muhula wa masomo utaanza rasmi tarehe **11/01/2021.**

Shule ya sekondari Chisano ipo katika kijiji cha Mgugwe kata ya Chisano kilometa 16 kutoka tarafa ya Mlimba.

Aidha napenda kukuarifu kuwa serikali kupitia waraka wake wa Elimu namba tano (05) wa mwaka 2015 imefuta michango yote. Pamoja na hayo utapaswa kuzingatia maagizo yafuatayo;

## 1. SARE YA SHULE.

- Sketi mbili (02) rangi ya ugoro kwa wasichana. Ziwe ndefu **kuvuka magoti!.**
- Suruali mbili (02) rangi ya ugoro kwa wavulana.Zisiwe **MODO** na zisiwe za kuvaa kwa mlegezo!.
- Mashati meupe mawili (02) mikono mifupi yenye uwezo wa kuchomekea.
- Viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi visivyo na urembo wowote vya kufunga kwa kamba.
- Soksi nyeupe jozi mbili(02). Ziwe ndefu.
- Kwa wasichana wa kiisilamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu inayofanana na sare ya shule.
- T-shirt zinapatikana shuleni kwa Tsh 10,000/= kwa atakaye hitaji.
- Sare ya michezo ni BUKTA ya bluu (kwa wavulana) na SKETI ya bluu kwa wasichana na T-SHIRT nyeusi kwa wote.
- Haitaruhusiwa kabisa mwanafunzi kuwa na sare ya mashono tofauti kama ilivyoelekezwa na shule kwenye fomu hii ya kujiunga na shule hii.

## 2. MAHITAJI BINAFSI KWA AJILI YA MASOMO (MZAZI ANUNUE MWENYEWE).

- Madaftari makubwa (counter book) yasiyopungua kumi na mbili (12).
- Kalamu za kutosha (peni na penseli).
- Mkebe wa vifaa vya hisabati (mathematical set).
- Kamusi (Dictionary) English – English.
- Mkoba mzuri wa kubebea daftari zako na vifaa vingine.
- Ndoo ndogo ya lita 10 kwa matumizi binafsi hasa wakati  ambapo shuleni hakuna maji.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotelewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni ( preparation).

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.2 **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule.**

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kusababisha mimba (wavulana).
12. Kugoma, kuchochea na kuongeza au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

## 4. UTARATIBU WA KURIPOTI NA USAJILI.

Usajili utafanyika shuleni kuanzia tarehe **04/01/2021** hadi **08/01/2021**.Fika kuanzia saa 2:00 asubuhi ukiwa na mzazi/mlezi wako. Hatua kali zitachukuliwa kwa yeyote atayeshindwa kuripoti shuleni kufikia tarehe **11/01/2021**. Mlete mwanafunzi aanze masomo hata kama maandalizi yatakuwa bado hayajakamilika. Fika shuleni na mzazi/mlezi ili kupata utaratibu. Masomo (siyo usajili) yataanza rasmi tarehe **11-01-2021.**

## 5. HALI YA AFYA MWANAFUNZI.

Utapaswa kwenda kupima afya kwenye hospitali yoyote ya serikali (siyo zahanati) ili kupata hali ya afya yako ili shule iweke utaratibu rafiki. (Fomu ya hospitali imeambatanishwa).

Ninakutakia maandalizi mema na yenye baraka ,ujipange kusoma kwa bidii.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI CHISANO

**EDUCATION – HEART OF LIFE.**

………………….

**LEONARD BAREMA HATUNGIMANA**

**MKUU WA SHULE.**

**NA.SIMU**; **0688011224 / 0758216386** – Mkuu wa shule.
**0786356684 / 0757545528** – Makamu mkuu wa shule.

**CHISANO SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**FROM THE HEADMASTER**
**CHISANO SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 164**
**MLIMBA**
**DATE ______________________**

**TO: THE MEDICAL OFFICER**
**_______________________**
**GOVERNMENT HOSPITAL.**

**NAME OF PUPIL ________________________________________________________________**

Please examine the above named pupil and arrange any necessary treatment so that the certificate can be signed and the pupil turn to the school on time.

A certificate signed by a certified medical officer at voluntary agency Hospital is acceptable so long as the bill is settled to the pupil himself/herself.

**_____________**
**HEADMASTER.**

**MEDICAL CERTIFICATE**
**TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER.**

Please examine the above named pupil with regard to.

Skin ……………………………………………………………………………………………………

Eye ………………………………………………………………………………………………………

Teeth ……………………………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………………………

Ears ……………………………………………………………………………………………………

Abdomen/Stood …………………………………………………………………………………………

Spleen ……………………………………………………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………………………………………………

H.B ( Haemoglobin ) ……………………………………………………………………………………

And I certify that;

(i) The pupil is in good health and free from infection diseases.
(ii) He or she is fit to continue with normal school routine.
(iii) Any other …………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

| | | | |
|---|---|---|---|
| …………………………………… | …………….. | …………………… | ……………………. |
| **NAME OF MEDICAL OFFICER** | **SIGNATURE** | **OFFICIAL STAMP** | **DATE** |